

KUBORESHWA KWA KILIMO CHA UMWAGILIAJI WA MPUNGA BAHI-DODOMA

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Mwezi Novemba mwaka 2016, Mradi wa LIC ulipokea pendekezo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kuwekeza katika kuboresha vifaa vya umwagiliaji na teknolojia ya uzalishaji katika mashamba matano ya mpunga, yaliyopo Bahi sokoni, Matajira, Uhelela, Nguvumali na Mtazamo, yote yapo wilaya ya Bahi mkoani Dodoma. Uwekezaji wa mradi wa LIC ulijumuisha msaada wa upangaji wa matumizi bora ya ardhi na umiliki kupitia matumizi ya gharama nafuu za teknolojia ya setilate na msaada wa kuanzishwa muundo wa usimamizi wa fedha ili kuhakikisha uendeshaji sahihi na matengenezo ya mipango na ukusanyaji wa mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.



Shamba la kilimo cha umwagiliaji cha Mpunga lililopo Mtazamo katika Wilaya ya Bahi

Miundombinu ya umwagiliaji ya shamba lililopo Matajira

Kabla ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ,usambazaji wa maji katika miradi mitano ya umwagiliaji ulikuwa duni na usio na uwiano, na kusababisha mavuno mabaya. Ukarabati umesababisha ongezeko la mavuno kwa 25% - 100%, muda unaonyesha pengo kubwa kati ya wakulima wenye ufanisi zaidi na wale wasio na ufanisi. Kwa muda mrefu dalili inaonyesha uwezo mkubwa wa kuongezeka kwa mavuno kwa mashamba yaliyo na mavuno kidogo kupitia kufundisha wakulima na kuanzishwa kwa teknolojia bora na kufanya kilimo cha kisasa.

Uwekezaji uliofanywa na mradi wa LIC haujabadilisha tu uzalishaji wa mpunga katika wilaya husika ya Bahi lakini umetumika kama kifungua jicho kwa wakulima wa mpunga na wawekezaji wengine wenye uwezo na wafanyabiashara wanaojihusisha na mnyororo wa thamani wa mpunga.



Moja ya machine za usindikaji wa mpunga wilayani Bahi



Baadhi ya maghala ya Mpunga wilayani Bahi



Mambo muhimu na mafanikio ya mradi

- Ongezeko la uzalishaji wa mpunga limetokana na miundombinu bora ya umwagiliaji na upanuzi wa ardhi ya kilimo cha umwagiliaji. Fursa mpya za ajira zimeundwa katika uandaaji wa vitalu,, kupandikiza, kupalilia, kuponda, kuhamisha mifuko/magunia, usindikaji na usafirishaji lakini pia katika biashara ongezeko la jumla la uzalishaji wa mpunga na kipato cha wakulima yamenufaisha jamii inayozunguka mashamba ya mpunga kiuchumi.
- Ongezeko la mavuno ya mpunga yamesababisha uwekezaji mpya kwenye maghala na katika vifaa vya usindikaji
- Kuongezeka kwa kipato cha kilimo na faida kumewafanya wakulima kutambua thamani ya kuwekeza zaidi kwenye uzalishaji na usindikaji wa mpunga. Wakulima wengi zaidi sasa wanahama kutoka kwenye kuuza malighafi za mpunga na kusindika mchele.
- Halmashauri ya Wilaya ya Bahi kupitia makubaliano na vyama vya wazalishaji sasa wametambua ongezeko wa ukusanyaji wa mapato ya shilingi 8,000 kwa kila kitalu.

Mradi wa LIC umewekeza shilingi milioni 239 kuboresha kilimo cha umwagiliaji wa mpunga katika Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

Septemba 2018